

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA KUMI NA SITA

30 APRILI, 2024



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA KUMI NA SITA – TAREHE 30 APRILI, 2024

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA KILIMO:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

WAZIRI WA MADINI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

202. MHESHIMIWA JOHN MARKO SALLU (HANDENI VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Afya Tarafa ya Kwamsisi – Handeni.

203. MHESHIMIWA ABUBAKARI DAMIAN ASENGA (KILOMBERO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kwa nini Wananchi wa Wilaya ya Kilombero wanatozwa Ushuru wa Mazao chini ya Tani Moja kinyume na maelekezo ya Serikali.

204. MHESHIMIWA DEUS CLEMENT SANGU (KWELA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini ahadi ya ujenzi wa Barabara ya Chombe hadi Kaoze - Kwela itatekelezwa.

205. MHESHIMIWA JACQUELINE KAINJA ANDREW (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga nyumba za Walimu nchini.

OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

206. MHESHIMIWA SAASHISHA ELINKIYO MAFUWE (HAI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu kuteketeza Miti ya Mkaratusi nchini baada ya tafiti kuonyesha inaharibu mazingira.

WIZARA YA MADINI:

207. MHESHIMIWA ASIA ABDUKARIMU HALAMGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha vifaa vyatya kuchimbia Madini ya Chumvi Wananchi wa Kata ya Gendabi - Hanang'.

WIZARA YA KILIMO:

208. MHESHIMIWA JAPHET NGAILONGA HASUNGA (VWAWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, upi mkakati mahsusini wa Serikali wa kutafuta masoko ya zao la Kahawa.

WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

209. MHESHIMIWA CECILIA DANIEL PARESSO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itafikisha mawasiliano ya simu katika Vijiji visivyo na mawasiliano - Karatu.

WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

210. MHESHIMIWA MWANAKHAMIS KASSIM SAID (MAGOMENI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, kuna mkakati gani ya kuhamasisha Timu ya Taifa ifanye vizuri katika AFCON 2027 kama inavyofanyika kwa Vilabu vya Yanga na Simba.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

211. MHESHIMIWA ATUPELE FREDY MWAKIBETE (BUSOKELO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali imejipangaje kukuza vipaji kwa Watanzania waliogundua Teknolojia mbalimbali hapa nchini.

WIZARA YA MAJI:

212. MHESHIMIWA KASALALI EMMANUEL MAGENI (SUMVE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itaanza kusambaza maji ya bomba kutoka Ziwa Victoria katika Vijiji vyote vya Jimbo la Sumve.

213. MHESHIMIWA AGNES ELIAS HOKORORO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Mabwawa ya Lukuledi na Mtambaswala yatajengwa - Mtwara.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

214. MHESHIMIWA TECLA MOHAMEDI UNGELE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itajenga Vituo vya Polisi Njinjo – Kilwa na Kibutuka - Liwale.

WIZARA YA AFYA:

215. MHESHIMIWA AMOUR KHAMIS MBAROUK (TUMBE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, lini Serikali italeta Sheria ya Kuzuia Uvutaji wa Sigara na mazao mengine ya Tumbaku hadharani.

WIZARA YA UJENZI:

216. MHESHIMIWA ZAYTUN SEIF SWAI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, Serikali haioni haja ya kujenga Daraja la Mto Athuman - Ngorongoro ili kunusuru maisha ya Wananchi nyakati za mvua.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MADINI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**DODOMA
30 APRILI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**